

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA**

Tel: Fax 025-2820068

Fax No. 025-2820068

Email: [ded@mpandadc.go.tz](mailto:ded@mpandadc.go.tz)

Website: [www.mpandadc.go.tz](http://www.mpandadc.go.tz)

S.L.P 1,  
**MPANDA.**



## **TAARIFA KWA UMMA**

Mwenyekiti wa kamati ya maafa ya wilaya ya Tanganyika Bw.Salehe Mhando amewakabidhi vyakula wahanga wa mafuliko yaliyotokea Februari 2, 2017 katika kijiji cha Isengule, Kata ya Isengule wilayani Tanganyika.

Vyakula vilivyokabidhiwa ni magunia 26 ya unga wa sembe wa kilo 25, maharagwe, mafuta ya kupikia, chumvi na sabuni. Jumla ya familia 26 zilikosa malazi baada ya nyumba zao kuanguka. Nyumba hizo zilijengwa kwenye mkondo wa maji yanayoelekea katika ziwa Tanganyika.

Vyakula hivyo vyenye dhamani ya shilingi 2,618,200 vimeonekana kuwa ni msaada mkubwa sana kwa wahanga hao. Ikumbukwe kuwa gunia moja la unga kilo 25 ni kati ya 43,000 na 45,000 na maharage kilo 10 kati ya 20,000 na 24,000. Kila familia ilipewa vitu vyenye thamani ya shilingi 100,700.

Hata hivyo mwenyeketi wa halmashauri ya wilaya ya Mpanda Mh. Hamad Mapengo alimshauri Mkuu wa wilaya kuunda tume itakayokuwa chini ya Mkurugenzi kufanya utafiti wa kina ili kubaini chanzo cha mafuliko hayo na kuondoa utata uliopo. Kuna baadhi ya wananchi wanasema mafuliko hayo yanetokana na vizibo 4 na wengine wanasema yanetokana na maji ya mvua yanayotoka Kafisha.

Sylvanus Ntiyakenye  
Afisa Habari na Uhusiano  
Halmashauri ya wilaya ya Mpanda.  
07/02/2017